



**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

**SHULE YA SEKONDARI TUMONA**

**S.L.P 8954, MOSHI, SIMU: 0753380229/0714731006**

TAREHE: 03/12/2020

**Kumb Na TSS/JNG/2021/VOL.15/FI**

**Mwanafunzi.....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUMONA WILAYA  
YA HAI, MKOA WA KILIMANJARO KIDATO CHA I MWAKA 2021**

**1.0. UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga **kidato cha kwanza** katika shule hii **mwaka 2021**. Shule ya sekondari Tumona ipo katika kijiji cha Orori, kata ya Machame-Narumu, umbali wa kilomita kumi na saba (km 17) ,kutoka mji wa Bomang'ombe ambayo ni makao makuu ya wilaya Hai.

**Muhula** wa kwanza wa masomo utaanza rasmi **tarehe 11/01/2021**. Unatakiwa **kuripoti** shuleni kuanzia tarehe **07/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/01/2021** saa 9:30 Alasiri

## **2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 Sare ya shule hii ni **brown mpauko** kwa wavulana na **Pink** kwa wasichana

### **(a) wasichana**

- Sketi mbili(2) za marinda ya kawaida ambazo zinavuka magoti(kitambaa kiwe namba 1 au grade 1 ili kisipauke)
- Mashati meupe mawili(2) ya mikono mifupi aina ya tomato(yawe mapya,kulingana na ukubwa wa mwanafunzi).
- Tai moja(1) Ya pink yenye miraba miwili,mmoja mweupe na mwingine wa pink
- Sweta moja(1) ya rangi nyeusi.
- Soksi jozi mbili(2) nyeupe aina stocking
- Viatu vyeusi, vya Kamba,visivyo na kisigino kirefu na vinavyoweza kupigwa kiwi

**NB. Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya shati (iwe nyeupe). Kwa wanafunzi wa kiislamu wanaweza kushona, 'short kanzu'**

### **(b) Wavulana**

- Suruali mbili(2) ndefu za rangi ya brown mpauko na ambazo hazibani(ambazo sio modo)
- Mashati mawili(2) ya mikono mifupi aina tomato(yawe mapya,kulingana na ukubwa wa mwanafunzi)
- Tai moja moja (1) ya rangi ya brown mpauko yenye miraba mwili,mmoja wenye rangi ya suruali na mwingine wenye rangi ya shati.
- Sweta moja(1) yenye rangi nyeusi
- Soksi jozi mbili(2) nyeusi
- Viatu vyeusi,vya ngozi,vyenye Kamba,visiwe na kisigino kirefu na viwe vinaweza kupigwa kiwi
- Mkanda wa suruali,mweusi usio na madoido

## **2.2. sare ya michezo ya shule hii ni:**

- (i) wavulana-Tracksuit ya rangi nyeusi
- (ii) wasichana-Tracksuit ya rangi ya bluu

Nb. Rangi na michoro ya sare hizi vimeambatanishwa na fomu hii. Sare zote zitakaguliwa siku ya kuripoti mwanafunzi.

## **3.0. VIFAA VYA DARASANI**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vya darasani kwa ajili ya masomo na mazoezi ya kitaaluma hapa shuleni kama ifuatavyo:

- (i) Madaftari makubwa 10(counter book Quire 3)
- (ii) Madaftari madogo 10,kwa ajili ya mazoezi
- (iii) Mathematical set(mkebe wa vifaa vya hisabati na sayansi)
- (iv) Kalamu za wino(nyeusi au bluu),penseli,rua ndefu na vifutio
- (v) Begi imara la kubebea madaftari na vitabu

## **Vifaa vingine ambazo mwanafunzi anatakiwa kuwa navyo ni vifuatavyo:**

- (i) Bakuli,kikombe na kijiko kwa ajili ya uji na chakula cha mchana
- (ii) Mwavuli kwa ajili ya kipindi cha mvua
- (iii) Buti kwa ajili ya matope kipindi cha mvua

## **4.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

4.1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na: 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu,sayansi na Mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya kusimamia elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Hivyo, unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule
- (f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- (h) Kutunza mali za umma

#### **4.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa masomo**

- (a) Uasherati na ushoga na vitendo vyote vinavyohusiana na kushiriki katika mapenzi ukiwa mwanafunzi
- (b) Ubakaji
- (c) Wizi
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile utumiaji wa bangi,cocaine,kubeli,ugoro,mirungi na kadhalika
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma,kama vile; kuandika katika kuta za majengo ya shule,kuharibu viti na meza kwa kuvunja au kuandika maandishi au michoro isiyo ya msingi,kuvunja vioo,mabomba na kadhalika
- (g) Kudharau bendera ya taifa
- (h) Kupata mimba au kusababisha mimba
- (i) Kuoau au kuolewa
- (j) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (k) Kugoma,kuchochea mgomo na kuongoza mgomo

- (l) Kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
- (m) Kumiliki,kukutwa,kutumia simu ya mkononi au laini ya simu(sim card) katika mazingira ya shule na kipindi chote ukiwa mwanafunzi katika shule hii.
- (n) Kufanya jaribio lolote na kujiua au kutishia kujiua kwa kunywa sumu na kadhalika
- (o) Kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa
- (p) Kutembelea au kukutwa katika majumba ya starehe au nyumba za kulala wageni
- (q) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
- (r) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,walimu,watumishi wengine,wazazi na jamii kwa ujumla.
- (s) Kutohudhuria masomo kwa siku tisini au Zaidi bila taarifa.

**5.0. MAMABO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI SIKU YA KURIPOTI**

- (a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi
- (c) Mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai
- (d) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule

NB. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

**BENJAMIN STEPHANO MTWEVE**

**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

**SHULE YA SEKONDARI TUMONA**

**S.L.P 8954, MOSHI**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

(Taarifa hii ijazwe na wanafunzi wote wa kidato cha kwanza na wanafunzi wanaohamia katika shule hii)

MAJINA MATATU YA MWANAFUNZI.....

TAREHE YA KUZALIWA.....URAIA.....

KABILA.....DINI.....DHEHEBU.....

JINA LA BABA.....HAI/AMEFARIKI

JINA MAMA.....HAI/AMEFARIKI

JINA KAMILI LA MLEZI (KAMA HANA WAZAZI).....

UHUSIANO NA MLEZI.....

KAZI YA BABA/MAMA/MLEZI.....

JAMAA KATIKA FAMILIA;

i. IDADI YA KAKA.....

ii. IDADI YA DADA.....

iii. YEYE NI WANGAPI KATIKA FAMILIA.....

ANWANI YA NYUMBANI.....SIMU YA MZAZI/MLEZI.....

ULEMMAVU WOWOTE WA VIUNGO/AKILI.....

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

**SHULE YA SEKONDARI TUMONA**

**S.L.P 8954, MOSHI**

**HATI YA KIAPO CHA UTII WA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

(Taarifa hii ijazwe na wanafunzi wote wa kidato cha kwanza na wanafunzi wanaohamia katika shule hii)

**A: MWANAFUNZI**

Mimi.....Nikiwa mwanafunzi wa shule hii,nakubali kuwa,umma wa nchi hii ya Tanzania,ndiyo uliyonipa nafasi hii maalumu ya masomo,ili nimalizapo Niweze kuitumikia nchi katika kuleta maendeleo. Hivyo basi ninahaidi kwamba,nitajibiidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ili kutimiza shabaha hiyo,ninakubali na kuhaidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri nitakazopewa na uongozi wa shule(walimu na serikali ya wanafunzi). Nikiwa na malalakimiko au maoni nitayafikisha kwa uongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila kuogopa.

**Tarehe..... Saini.....**

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi bwana/bi.....mzazi/mlezi wa .....

Nimesoma kwa makini sheria za shule kama zilivyoandikwa katika maagizo kwa wazazi/walezi na nazikubali sheria hizo na nitashirikiana na shule kuona kuwa mwanangu anazingatia kwa makini kwa manufaa ya umma. Endapo atakiuka,adhabu stahiki zichukuliwe kulingana na miongozo,

**Tarehe..... Saini.....Simu.....**



**TUMONA SECONDARY SCHOOL**

**P.O.BOX 8954, MOSHI. MOBILE: 0753380229/0712884140**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**PART I: PERSONAL PARTICULARS (To be filled by the student)**

Surname.....Other names.....Form.....

Sex.....Age.....Headmaster's name.....Signature.....Stamp.....

**PART II: PERSONAL HISTORY** (To be filled in a government hospital by qualified medical officer)

Are you suffering or have suffered from any of the following? Indicate Yes or No

- |                                    |                                     |
|------------------------------------|-------------------------------------|
| 1. Tuberculosis.....               | 11. Asthma .....                    |
| 2. Rheumatic fever.....            | 12. Allergic disorder.....          |
| 3. Heart diseases.....             | 13. Gastric or duodenal ulcers..... |
| 4. Jaundice.....                   | 14. Dysentery.....                  |
| 5. Kidney disease.....             | 15. Gynecological disorder.....     |
| 6. Epilepsy.....                   | 16 .Deformity.....                  |
| 7. Mental illness.....             | 17. Eye disorder.....               |
| 8. Ear, Nose, throat disorder..... | 18 .Skin disease.....               |
| 9. Anemia.....                     | 19. Varicose vein.....              |



10. Diabetes..... 20. Any other serious disorder (specify).....

**PART III: PHYSICAL EXAMINATION**

1. Height (cm).....Weight (kg).....Skin.....

2. Eye. Conjunctive..... Pupil.....

3. Vision. Right.....Left.....

4. Ears (state if any discharge).....

5. Mouth/throat.....

6. Nose.....

7. Respiratory system.....

8. Abdomen.....

9. Any abnormality.....

10. Cardiovascular system.....

11. Blood pressure.....

12. Systolic.....

13. Diastolic.....

14. Heart. Any murmur.....

15. Arteries veins.....

**PART IV: LABORATORY EXAMINATION**

1. Urine.

Albumin..... Sugar.....Leucocytes.....schistosoma.....

2. Stool. Special emphasis on hookworms or Schistosoma.....

3. Blood examination

(a) Hb level.....

(b) Neutrophil.....

(c) Eosinophils.....

(d) Basophiles.....

(e) Lymphocytes.....

(f) Monocytes.....

(g) ESR.....

4. E-RAY EXAMINATION: Chest (includes radiologist’s report).....

5. Serology widal test.....VDRL.....

6. PREGNANCY TEST (For girls).....

**PART V: CONCLUSION**

I have examined Mr/Miss.....and consider that she/he is physically and mentally fit/not fit to be admitted for secondary education.

Name.....Tittle.....Qualification.....

Signature.....Date.....Address.....official stamp.....